JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI ILEJE,
138
BARABARA YA ILEJE SEKONDARI
S.L.P 124,
54301
**ITUMBA-ILEJE**
24/04/2024.

SIMU NO.
MKUU WA SHULE: **0757-579877/ 0678 579 877**
MAKAMU MKUU WA SHULE: **0757487618/ 0624 380 419**
MATRON/PATRON **0764 326 443**

MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI ………………………………………………………………
S.L.P……………………………………….
……………………………………………….

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ILEJE HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE MKOA WA SONGWE MWAKA 2024/2025.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2024/2025 tahususi ya………….. Shule ya sekondari Ileje ipo umbali wa km 04 Kutokea makao makuu ya Wilaya Kusini mwa kijiji cha Itumba usafiri wa basi kutoka mjini Ili uweze kufika shuleni ukitokea STANDI KUU Mbeya, utapanda gari zinazoenda Tunduma na kushuka standi ya Mpemba. Ukitokea DSM utapanda gari zinazoenda Tunduma na utashukia standi ya Mpemba. Kwa wale wanaotoka njia ya Sumbawanga nao watashukia standi ya Mpemba. Kutoka standi ya Mpemba utapata usafiri wa kwenda Itumba ambayo ndiyo makao makuu ya wilaya ya Ileje. Aidha upo usafiri wa moja kwa moja kutoka Mbeya (Stend ya Airport ya zamani) ambapo kuna Mabasi yanayoanza safari zake hapo hadi Ileje, utashukia kituo cha Ileje Sekondari. Nauli ya kutoka Mbeya hadi Ileje ni Tsh 8,000/=.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **…………..** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………….

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**

2.1 Sare ya shule








T-SHIRT-NJANO

### A. WAVULANA

a) **Suruali 2 za kitambaa, moja rangi ya kahawia (brown) isiwe rangi ya ugoro(tobacco), na ya pili iwe rangi nyeusi.** Mfano wa kitambaa umeambatishwa hapo juu. Mshono wa suluari chini isipungue 14
**b)** Mashati 2 yote rangi nyeupe mikono mirefu yawe marefu ya kuweza kuchomekea kwenye suruali vizuri (uje nayo).
**c)** Tai 2 ndefu rangi ya vitambaa vya suruali hapo juu.
**d)** Viatu vyeusi vya ngozi, jozi 2 vyenye visigino vifupi na vya kamba na pia visiwe na mapambo aina yoyote.
**e)** Soksi rangi nyeusi jozi mbili.
**f)** Sweta rangi ya **Ugoro (Tobacco**) **Siyo Brown au Kahawia** iliyoshonwa vizuri yenye shingo ya "V" shingoni
**g)** Mkanda mweusi wa ngozi.
**h)** Raba za michezo nyeusi (zitakaguliwa)
**i)** Nguo za michezo T-shirt na kaptula za rangi ya bluu (zitakaguliwa)


### B. WASICHANA

a) Sketi 2 za vitambaa, moja rangi ya kahawia (brown) **isiwe rangi ya ugoro(tobacco),** na ya pili iwe nyeusi. Mshono wa sketi ni marinda ya kawaida yenye rinda pana moja mbele na nyuma, iwe ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguuni chini ya goti.
**b)**
**c)** Mashati 2 yote rangi nyeupe zenye mikono mirefu.
**d)** Sweta rangi ya **Ugoro (Tobacco**) **Siyo Brown au Kahawia** iliyoshonwa vizuri yenye shingo ya "V."
**e)** Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi, vya kamba na visiwe na mapambo yoyote.
**f)** Tai 2 ndefu rangi ya kitambaa cha sketi za hapo juu.
**g)** Soksi ndefu rangi nyeupe jozi mbili.
**h)** Raba za michezo nyeusi (zitakaguliwa)
**i)** Nguo za michezoT-shirt na kaptula za rangi ya bluu (zitakaguliwa)
j) Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

NB: Aidha lipo vazi la kazi za nje maarufu kwa "Shamba dress" ambalo huvaliwa na wanafunzi wanapokuwa katika kazi za mikono nje ya masomo na pia vazi hilo hutumika kama nguo anayovaa akiwa shuleni, sare hizo zishonwe kwa mashono yaliyoonyeshwa katika michoro hii hapa chini idadi ya aina hiyo ya sare zisipungue mbili (02).

### A. WASICHANA

- Truck suit rangi ya blue yenye mistari ya mieupe.
- Gauni draft ndogo ndogo zenye rangi ya kijani na nyeupe (angalia mfano wa kitambaa kimeambatanishwa na barua hii).



Marinda ya kupanga

Gauni la kuvaa wakati wa kazi na usio wa kazi maeneo ya shule (shamba dress) gauni liwe refu mpaka kwenye kifundo cha mguuni.

- Mwanafunzi aje na T-shirt rangi ya njano yenye kola nyeusi, kama hutapata maeneo ulipo zinapatikana shuleni kwa Tsh 16,000/=.

**B. WA VULANA**

- Truck suit rangi ya blue yenye mistari ya mieupe.
- Suruali khaki mbili (2) – mashono kama suruali ya sare ya shule.
- Mwanafunzi aje na T-shirt rangi ya njano yenye kola nyeusi, kama hutapata maeneo ulipo zinapatikana shuleni kwa Tsh 16,000/=.

Ili kuepuka kuchanganya rangi ya ugoro na kahawia vitambaa vya sketi na suluari vitapatikana shuleni.

NB:

- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni kumiliki simu shuleni au kutumia, mawasiliano yote yafanyike kupitia namba ya Mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule, na Matron/patron
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za ziada/ kuvaa au kupatikana na mavazi ya aina nyingine yoyote ya kiraia nje na sare au shamba dress au track suit kama ilivyoainishwa hapo juu.
- Atakayepatikana na simu au mavazi tofauti na hapo juu akiwa amevaa shuleni au ametunza Bwenini atapewa adhabu kali ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

## 2.2 Michango ya shule

(i) Mchango wa uendeshaji wa shule 65,000/=
(ii) Tahadhari 5,000
(iii) Nembo 5,000
(iv) Kitambulisho 5,000

**Jumla 80,000/=**

Michango hii itumwe kwenye akaunti ya shule

**NMB Account No. 60801200054 ILEJE SEKONDARI RECURENT EXPENDITURE). Angalizo:** Jumla ya michango yote ni **Tsh 80,000/=** Pia hakuna michango itakayopokelewa kwa fedha tasilimu shuleni.

2.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni

(i) Laboratory coat (kwa wanafunzi wote wa masomo ya Sayansi)
(ii) Ream ya karatasi A4 - **2** (kwa muhula)
(iii) Rulled paper moja – **01 (**kwa muhula)
(iv) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia (itakaguliwa).
(v) Scientific calculator kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi
(vi) Godoro futi 2 $^{1/2}$
(vii) Mashuka pair 2 (rangi ya bluu bahari), blanketi 1, foronya1(bluu bahari) chandarua 1
(viii) Bima ya Afya ni lazima kwa wanafunzi wote, Kwa wasio kuwa na Bima ya Afya njoo na Tsh 10,000/= kwa ajili ya kufungulia bima.
(ix) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe) (vitakaguliwa)
(x) Ndoo mbili, kubwa 1(lita 20) na ndogo 1 (lita 10)
(xi) Jembe1lenye mpini (kwa wote)
PCM – shoka moja lenye mpini, Driyer(squzer) moja na mfagio laini (soft broom)
PCB – panga moja, Driyer (squzer) moja na mfagio mgumu (hard broom)
HGK – Driyer (Squzer) 1, na brash za chooni 2
HGL – mfagio laini (soft broom), Driyer(squzer) 1na fyekeo moja
HKL – mfagio mgumu (hard broom), Driyer(squzer) 1 na shoka moja lenye mpini

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku ( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

3.2 **Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na**:

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 mfululizo bila taarifa/ utoro
(iii) kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lungha chafu kwa mwanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(vii) Kufuga ndevu
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(ix) Uvutaji wa sigara
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi
(xix) Kumiliki na kutumia simu pamoja na vifaa vyake shuleni.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne(4) za passport size za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule …0757 579 877
- Makamu Mkuu wa Shule ……0757 487 618
- Mwandamizi Taaluma … 0755 143 486
- Mwandamizi Malezi … 0762 231 119

*KARIBUNI SANA ILEJE SEKONDARI*

………………………………….

JULITHA T. MWAULAMBO
MKUU WA SHULE
0757579877

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI ILEJE
ILEJE-SONGWE

**<u>SHULE YA SEKONDARI YA ILEJE</u>**
**<u>FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE</u>**

1. **Sehemu ya mwanafunzi**

Mimi ………………………………. Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha kwanza/tano ………………….. Katika shule ya Sekondari ya Ileje na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea.

Anuani yangu ya kudumu ni ………………………………………………………….

……………………………………………………………..
……………………………………………………………..
……………………………………………………………..

**2. Sehemu ya Mzazi/Mlezi**

Mimi ………………………………… ninakubali mtoto wangu ……………………….
Kuchukua nafasi kuingia Ileje shule ya sekondari kidato cha ………..
Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule Kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.
Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa.
Anuani yangu ya kudumu ni:-

…………………………………………………
…………………………………………………
…………………………………………………
…………………………………………………

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi.
Sahihi………………………………….. Tarehe …………………

**SHULE YA SEKONDARI ILEJE**
**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina lako kamili lilivyotumika kidato cha nne…………………………………….. 
   Dini yako/dhehebu ……………………………………………………………….
2. Jina kamili la baba mzazi/mlezi ………………………………………………….
   Kazi yake ……………………………………………………………………………
   Anwani kamili ya baba mzazi/mlezi ………………………………………………
   Na. yake ya simu ya mkononi ……………………………..
   Na. yake ya simu ya mezani ……………………………….
   Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi: Mkoa ……………….. Wilaya …………….
   Tarafa ……………………………………… Kata ………………..Kijiji/Mtaa………..
3. Jina kamili la mama mzazi/mlezi …………………………………………………..
   Kazi yake ……………………………………………………………………………..
   Anwani kamili ya mama mzazi/mlezi …………………………………………….
   Na. yake ya simu ya mkononi ……………………………….
   Na. yake ya simu mezani ……………………………………..
   Mahali anakoishi mama mzazi/mlezi: Mkoa …………………Wilaya …………….
   Tarafa …………………………………Kata ………………….. Kijiji /Mtaa…………..
4. Majina ya watu watano wanaoruhusiwa kumtembelea/kumchukua mtoto wako.

| **Na.** | **Jina lake** | **Uhusiano** | **Mahali anakoishi** | **Anwani na namba yake ya simu** |
|---|---|---|---|---|
| 01 | | | | |
| 02 | | | | |
| 03 | | | | |
| 04 | | | | |
| 05 | | | | |

5. **shule nilizosoma msingi hadi kidato cha nne**

| **Na** | **Jina la shule** | **Darasa /Kidato** | **Kuanzia mwaka hadi mwaka** | **Mkoa** | **Wilaya** | **Kijiji/Kata** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **01** | | | | | | |
| **02** | | | | | | |
| **03** | | | | | | |
| **04** | | | | | | |
| **05** | | | | | | |

Namba yangu ya mtihani wa kidato cha nne …………………………..

**6. Matokeo yangu ya mtihani wa kidato cha nne**

| **Na.** | **Somo** | **Daraja** | **Na.** | **Somo** | **Daraja** |
|---|---|---|---|---|---|
| **01** | | | | | |
| **02** | | | | | |
| **03** | | | | | |
| **04** | | | | | |
| **05** | | | | | |
| **06** | | | | | |
| **07** | | | | | |
| **08** | | | | | |
| **09** | | | | | |
| **10** | | | | | |

Nilipata divisheni ………………….. Point ……………………..

7. Tarehe niliyoripoti hapa Ileje Sekondari ni ……………………...

   Masomo nitakayosoma ni:-

   1. ……………………….  2. …………………………  3. ……………………..

   4. ……………………….  5. ………………………….. 6. ……………………..

   Matarajio yangu baada ya kuhitimu masomo yangu mfano kuwa Daktari, Mwanasheria n.k

   1. ……………………………………………………………………………

   2. …………………………………………………………………………

   3. ……………………………………………………………………

   Hapa shuleni ningependa nijiunge na

   1. Michezo (i) ……… …………(ii) ………………………(iii)……………………………

   2.Kikundi cha utamaduni wa …………………………………………………..

   3. Mradi wa ………………………………………………………………………….

8. Taja kipaji maalumu ulichonacho na ungependa kukiendeleza:-

   ………………………………………………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………………

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENTS**

ILEJE SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 124,
**ILEJE**

**DISTRICT MEDICAL OFFICER**
**P.O.BOX …………..**
**…………………………**

**Dear Sir/Madam.**

**Re: A REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine Mr./Miss ……………………………………… as to his/her physical and mental fitness for admission as a Form Five Student at Ileje secondary school in the year 2014.

Yours sincerely,

**…………………..**
**HEADMISTRESS**

---

The Headmaster/The Headmistress,
I have examined Mr./Miss ……………………………as shown below and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full time secondary education.

1. Vision with/without glasses. Right …………………… left …………..
2. Blood pressure ………………………………… Haemoglobin …………..
3. Hearing …………………………………………….
4. Urine (a) Albumen ………………………….. (b) Sugar ……………………
5. (a) Venerial diseases ………………………..(b) Bilharzia ………………
6. Pregnancy ……………………………………………………………….
7. Neurosis ……………………………………………………………….
8. Is there any abnormality of:-
   (a) The heart ………………………………. (b) Lungs ……………………
   (c) The spleen ………………………………
9. Are there any serious diseases e.g. leprosy, epilepsy, asthma, diabetes etc.

Any comments ……………………………………………………………….

Date: ……………………………….. ………………………

Signature of Medical Officer

Station:………………………….. Designation: ………………..